**HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI**

**TANGAZO LA ZABUNI**

**Tarehe 10/12/2025**

Kamati ya CAMFED ya Wilaya ya Pangani (CDC), inayosimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya pangani na Shirika la **CAMFED**, inawaalika wafanyabiashara mbalimbali wenye uwezo wa kutoa huduma na vifaa vinavyohitajika kushiriki katika mchakato wa kuidhinishwa kwa ajili ya kutoa huduma hizo kwa mwaka **2026/2028**.Watoa huduma watakaoidhinishwa kupitia mchakato huu wataingizwa kwenye orodha ya wazabuni watakaoshindanishwa wakati wa manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali zinazohitajika katika utekelezaji wa miradi.

Tangazo hili linawahusu watu binafsi, kampuni, vikundi au taasisi zote zilizosajiliwa kisheria na zenye uwezo wa kutoa huduma au bidhaa husika kulingana na mahitaji ya miradi ya maendeleo.

Vifaa na huduma zinazohitajika vimeorodheshwa katika jedwali hapo chini.

| Na. | Vifaa/huduma | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Pakeji za Mikutano | Kumbi za mikutano, vifaa vya kuandikia, Chakula na vinywaji |
| 2 | Malazi – Hoteli na Nyumba za Wageni | Hoteli, Hosteli n, k, |
| 3 | Malazi na Huduma za Mikutano | Kuanzia watu 20 na kuendelea |
| 4 | Huduma za Chakula na Vinywaji | Kwenye mikutano mbalimbali |
| 5 | Vifaa vya Kuandikia na Vifaa vya Usafi | Daftari, Notebooks, Peni, Fagio, Sabuni za kufanyia usafi, n. k |
| 6 | Sare za shule, Mashuka, na Mablanketi | Shati, sketi, suruali, kaptula,Hijabu n. k |
| 7 | Huduma ya Kukodisha Magari | Magari aina ya Hard top |
| 8 | Samani za Ofisi | Meza, Viti, Kabati n.k |
| 9 | Matengenezo, Ukarabati na Huduma kwa Magari | |
| 10 | Baiskeli kwa Matumizi ya shule | Baiskeli aina ya Sehewa au Buffalo |
| 11 | Usafirishaji wa Mizigo na Shehena | |

| | | |
|---|---|---|
| 12 | Vifaa vya Jikoni na Mahitaji ya Kila Siku | Vyombo vya jikoni, Sukari, Maziwa,majani ya chai, n.k |
| 13 | Magodoro kwa Wanafunzi | Godoro la shule 2.5x6x3 |
| 14 | Vyandarua vya Kujikinga na Mbu | umbo la mstatili (mraba), vinavyofaa kwa vitanda vya wanafunzi katika shule za bweni. |
| 15 | Huduma za Uchapishaji – Vitabu, Mabango na Vifaa vya Matangazo | |
| 16 | Pedi za Kike kwa Wasichana Shuleni | |
| 17 | Viatu kwa Watoto wa Shule | Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba |
| 18 | Taa za Umeme wa Jua kwa Wanafunzi | |
| 19 | Vifaa vya Ofisi na Shule (Karatasi, Kalamu, Cartridge, Daftari n.k.) | Ream, Cartridge,Daftari za Msomi, Counter Books n. k |
| 20 | Wasambazaji wa Maji Safi | Kuanzia Litre 10 n.k |
| 21 | Ugavi wa Pembejeo za Kilimo | Mbolea, Mbegu mbalimbali, dawa za kuua wadudu n. k |
| 22 | Wauzaji wa Vifaa vya Ujenzi kwa Ajili ya Ukarabati wa Ofisi | Saruji,rangi,Mbao, fundi wa ukarabati wa ofisi |

**Zingatio.**

**Waombaji wote wanapaswa kuzingatia yafuatayo:**

1. Kujaza fomu ya kuomba kuwa mzabuni inayopatikana katika ofisi ya Afisa Elimu wa Wilaya-Sekondari na kuambatanisha pamoja na barua ya maombi. Fomu hii inatolewa **BURE.**

2. Muombaji awe na uzoefu wa kufanya kazi na Taasisi za Serikali ama Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs) na aorodheshe taasisi ambazo umefanya nazo kazi miaka ya karibuni.

3. Muombaji awasilishe maombi kwa **Afisa Elimu wa Wilaya-Sekondari P.O. Box 89 Pangani** Au **Ofisi ya CAMFED Wilaya Pangani** iliyopo Halmashauri ya zamani Pangani akiambatanisha:

i. Nakala ya uhalali wa kisheria (Power of Attonery) kwa muombaji ambaye ni kampuni.

ii. Nakala ya vyeti vya usajili wa kampuni/Ushirika/Vikundi.

iii. Nakala ya uthibitisho wa ulipaji kodi ya mwaka 2025 (Tax Clearance), cheti cha VAT, TIN na leseni halali ya biashara au huduma husika.

iv. Taarifa za benki (Jina la account na namba ya account).

4. Maombi yatapokelewa kuanzia Tarehe **15/12/2025** Mpaka Tarehe **10/01/2026. Maombi yote yatakayotumwa baada ya tarehe hizo hayatapokelewa.**
5. Mwombaji anaruhusiwa kuomba kutoa huduma/kusambaza bidhaa zaidi ya moja kati ya zilizoainishwa ikiwa ana vielelezo vya kuthibitisha kufanya biashara husika na kila huduma iombwe tofauti.
6. Kila ombi lijazwe vizuri na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain), ifungwe kwa nakiri, (SEALED) na juu ya bahasha iandikwe **MAOMBI YA KUWA MTOA HUDUMA -CDC.**
7. Muombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima.
8. Watoa huduma watakaochaguliwa watajulishwa kwa barua na watatakiwa kujaza fomu ya maadili (Code of conducts) na kuzirudisha kwa Afisa Elimu-Wilaya/ Mwenyekiti wa CDC.
9. Watoa huduma wasiochaguliwa watajulishwa kwa barua pia.
10. Waombaji wote wawe ndani ya mkoa husika.

**N: B; Maombi yote yatumwe kwa mwenyekiti wa CDC ambaye ni Afisa Elimu wa Sekondari wa Halmashauri au yawasilishwe kwenye ofisi ya CAMFED Wilaya ya Pangani.**

Imetolewa na

AFISA ELIMU
ELIMU YA SEKONDARI
WILAYA YA PANGANI

Lucy N. Gurtu

MWENYEKITI WA CDC WILAYA YA PANGANI

Kny: KAMATI YA CAMFED WILAYA YA PANGANI.